# KITABU CHA TAASISI ZA WENYEJI

Dr. Stephen Gibson

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki 2022 Shepherds Global Classroom
Haki zote zinahifadhiwa. Kuwasiliana na SGC, au saidia maono haya muhimu, nenda, go to: www.shepherdsglobal.org.

# Yaliyomo


Matumizi ya kitabu hiki kwa mafunzo ........ 5

(1) Umuhimu wa Mafunzo ya Huduma kwa Wenyeji ........ 7

(2) Utangulizi wa Shepherds Global Classroom ........ 13

(3) Sifa ya Mwalimu Mtarajiwa ........ 17

(4) Kuwaelewa Washiriki Wetu ........ 21

(5) Mbinu za Ufundishaji Mzuri ........ 25

(6) Jinsi ya Kufundisha Masomo ya SGC ........ 29

(7) Kugundua Walimu ........ 31

(8) Kuendesha Taasisi ya Wachungaji wenyeji ........ 35

Rasilimali za SGC Mtandaoni ........ 40

Maelezo ya Masomo ya Shepherds Global Classroom ........ 41

# Matumizi ya Kitabu hiki kwa Mafunzo



Kimsingi kitabu hiki ni mwongozo rejea wa wakufunzi, wasimamizi, na walimu wenyeji. Kwa wakati mwinigine wakufunzi wanaweza kukitumia kitabu hiki, kufunzia walimu na wasimamizi katika taasisi za wenyeji. Pia kwa wakati mwingine, sehemu fulani ya somo yaweza kutumika kufunzia mada husika au kutambulisha Shepherds Global Classroom (SGC).

Kitabu chote kinaweza kufundishwa kwa muda kama wa masaa sita katika kipindi cha mafunzo. Mara kwa mara wakufunzi wanapaswa kutoa nafasi ya mijadala darasani.

Washiriki wa mafunzo wanahitajika kuwa na Biblia, na daftari la kuandika, na kupata nakala ya kitabu hiki.

Wakufunzi wanapaswa kuja na vitabu mbalimbali vya masomo ya Shepherds Global Classroom kwa ajili ya wanafunzi kuyatathmini. Darasa linahitaji ngalau nakala tatu za vitabu vya masomo tofauti ili washiriki waweze kufanya mazoezi ya kufundishana katika vikundi vya watu watatu watatu.

Wakufunzi wakimaliza kufundisha hadi Sura ya 6, washiriki wanapaswa kuangalia vitabu vya masomo ya SGC. Wanapaswa kuangalia mwelekeo wa masomo hayo ulioko mwanzoni mwa kila kitabu cha somo. Washiriki wanapaswa kujadiliana kuhusu mwelekeo na kuhakikisha wanaelewa.

Mifano na mazoezi ni muhimu kwa mafunzo. Mkufunzi anaweza kuonyesha mfano wa jinsi ya kufundisha kwa kufundisha masomo matatu katika vitabu vya masomo. Mfano utakuwa mzuri endapo kila somo litatoka katika kitabu tofauti cha somo. Kama kuna mkufunzi zaidi ya moja au baadhi ya washiriki wenye uelewa, wanaweza kufundisha baadhi ya masomo ili kuonyesha mitindo mbali mbali.

Baada ya kuangalia mfano, mshiriki wa masomo haya anahitaji kufanya mazoezi ya kufundisha kwa vitendo.

Kwa kiwango cha chini mazoezi yanaweza kupangwa hivi: Wagawe washiriki katika vikundi vya watu watatu. Kila mshiriki katika kikundi atafundisha somo kwa wenzake wawili kwa muda usiopungua dakika 30. Kila moja wa washiriki wote watatu watafanya mazoezi na kuangalia ufundishaji wa wenzake wawili katika kipindi cha dakika 90.

Namna nzuri ni kuwa na siku ya mafunzo ya ziada iliyotengwa kwa ajili ya mazoezi ya vitendo vya washiriki kukiwa na mrejesho kutoka mkufunzi na washiriki wengine. Siku ya mazoezi haya inaweza kupangwa siku ya mwisho. Washiriki wanaweza kupata muda wa ziada ili wajitayarishe.

# Sura ya 1
# Umuhimu wa Mafunzo ya Huduma kwa Wenyeji

## Utangulizi

**Kanisa linapaswa kufundisha**. Yesu aliliambia kanisa kwenda mahali pote kufundisha amri zake (Mathayo 28:19). Paulo alisema kuwa Mchungaji anapaswa kuwa na uwezo wa kufundisha (1 Timotheo 3:2). Mafundisho haya ni sehemu ya kazi ya kufanya wafuasi. Kanisa linafundisha watu jinsi ya kuishi kama waamini, wanaoishi kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Mafundisho haya yanapaswa kufanyika kila mahali ambapo kuna waamini. Ki-mkakati makanisa yenye nguvu yanatayarishwa kwa ukweli wa kibiblia na mbinu za kivitendo ili kufundisha watu wao.

**Kanisa linapaswa kufundisha.**

> Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine (2 Timotheo 2:2).

Ulazima wa kufundisha huleta ulazima wa mafunzo ya huduma. Paulo alimwambia Timotheo kufundisha watu watakao fundisha wengine (2 Timotheo 2:2). Mafunzo sio suala la kufundisha maarifa tu. Mafunzo sio tu unafundisha waamini kwa faida yao. Mafunzo yanatayarisha waamini kusaidia watu wengine.

Yesu alitoa kipaumbele katika mafunzo ya huduma. Mwanzoni wa huduma yake, alichagua watu wachache ambao wangeweza kuongoza na kupanua kanisa. Hakutumia muda wake wote kuhubiria makutano ya watu; badala yake tunaona mara nyingi alitumia muda wake kufundisha viongozi kumi na wawili. Alipanua huduma yake kupitia wale ambao aliowafundisha.

**Shepherds Global Classroom hutoa mafuzo yanayoweza kutumiwa na huduma za wenyeji katika mazingira mbali mbali.**

## Kusudi la Mafunzo ya Huduma za Wenyeji

### Kufunza Wachungaji

Wachungaji wanapaswa kufunzwa itikadi, kutafsri Biblia, kuhubiri, na mbinu za kufanya wafuasi. Maelfu ya makanisa duniani kote yanaongozwa na wachungaji walio na vitabu vichache na wasio na mafunzo maalumu. Wachungaji wengi hawana mafunzo na hawana uwezo kuwafundisha wengine.

Wengi wa wachungaji duniani kote hawawezi kwenda chuo cha Biblia. Sio rahisi kwao kuacha familia, ajira, na huduma ili waende kwenye mafunzo mahali fulani kwa miaka kadhaa. Hawa wanahitaji mafunzo mahali waliko.

## Kufunza Washuhudiaji

Mtu yeyote ambaye amejionea neema ya Mungu iokoayo kwenye maisha yake anazo sifa za kueneza injili. Watu wanaweza kusema kile ambacho Mungu amewafanyia. Shuhuda zao zaweza kuwa na ushawishi, hususani kwa watu ambao wanawajua na kuona mabadilio yaliyotokea katika maisha yao.

Hata hivyo, wakati fulani mtu anaweza kuwa hana uwezo wa kuelezea mambo ya msingi yanayohusu injili. Kama wasikilizaji wako tofauti na hawamjui mtoa ushuhuda, wanaweza wasielewe ni jinsi gani wanavyoweza kupata mabadiliko ya aina hiyo.

Hata mtu ambaye amekuwa mwamini kwa miaka mingi anaweza kujiona hawezi kushuhudia watu wa jamii yake kwa sababu hawezi kujibu maswali yanayohusu ukristo. Mwamini huyu anajua jinsi alivyookoka, anavyojisikia anapoabudu, na jinsi ya kushirikiana na wengine katika mwili wa Kristo lakini hana uwezo wa kuelezea mambo hayo.

Wakati mwingine jamii ina uadui na Ukristo. Wakati mwingine wanaheshimu wafuasi wa Kristo ambao wanaishi maisha mema, lakini hata hivyo wanahitaji pia kusikia ufafanuzi wa Imani ya kikristo.

Mtu anaweza kuwa mshuhudiaji mwenye ufanisi kwa kujifunza kanuni za injili na itikadi za msingi zinazo kubalina na injili.

## Kulinda Kanisa

Wachungaji wanawajibika kulinda makanisa yao kwa mafundisho sahihi (Tito 1:9-14). Makanisa ya uongo na dini za uongo hutumia fikira zinazochanganya na kuhadaa watu. Ni huzuni kuwa watu wengi ambao walikuwa wameokoka baadaye hupotoshwa na kuchukuliwa na kanisa la uongo.

Mchungaji anapaswa kufundisha itikadi za kibiblia ili watu wajengwa katika Imani. Mafundisho lazima yawe yenye makusudi, yenye mpangilio na yenye kutolewa katika viwango mbalimbali ngazi ili kuwafikia watu wote wa kanisa.


## Kupanua Timu ya Huduma

Timu za michezo huwa zina mabenchi ya wachezaji ambao wakati wote hawachezi. Wengine wanaweza kuwa bado ni wadogo na wana ujuzi kidogo kuliko wale waliobobea, lakini wako katika mafunzo. Wengine wana uwezo maalumu utakaohitajika wakati fulani.

Kanisa lenye afya, linalokua linapaswa kuwa na “benchi”. Ni kosa kufikiri kuwa kwa sababu nafasi za uongozi kanisani zina watu, basi timu imekamilika. Huduma hufikia mwisho na haiendelei kukua isipokuwa kuna viongozi wanaosaidia kuanza aina nyingine ya huduma.

Kanisa lenye afya linapaswa kuwa na watu kwenye "benchi" ambao wanaendelezwa na wanafanyizwa mazoezi. Hilo linahitaji mafunzo ya kanisa la mahali. Kwa hiyo, huduma ya mafunzo sio tu ni ya watu wanashikilia nyadhifa.

Kazi ya mchungaji ni kuhakikisha mafunzo yanafanyika. Mchungaji hatakuwa na uwezo kutoa mafunzo yote mwenyewe, lakini anapaswa kuyapanga na kutia moyo. Anahitaji timu ya watu wanaotumika katika huduma mbalimbali kanisani.



> Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo (Waefeso 4:11-15).

Mungu huwapa watu wa kanisa la mahali karama na vipawa vinavyohitajika kutimiza kazi ya kanisa. Hivyo lazima kanisa lichukue wajibu wa makusudi kuendeleza watu.

**Kuimarisha Kanisa la Wenyeji**

Kanisa la wenyeji linaongozwa na watu wake, na ni miliki yao. Halitegemei kupata fedha au kuongozwa kutoka nchi za nje. Uimara wa kanisa la wenyeji ni muhimu kwa ajili ya afya na ukuaji wa makanisa.

Kanisa la wenyeji liko nyumbani katika utamaduni wake. Hili sio kanisa la nchi za nje.

Kanisa la faida kubwa wenyeji lina manufaa mengi:

1. Lina eneza injili kwa ufanisi na kuwafanya watu kuwa wafuasi katika utamaduni wao.
2. Kusanyiko linakuwa komavu na linatenda kazi kama mwili wa Kristo bila kutegemea nchi za nje.
3. Viongozi wake hujijenga na kufikia uwezo unaohitajika.
4. Washirika wa hapo huwezesha na huwajibika kwa ajili ya kazi ya huduma.

Baadhi ya makanisa ya wenyeji hayana afya kwa sababu yanakosa uimara wa itikadi na viwango vya maisha ya kikristo. Yanashindwa kushawishi jamii zao kwa ushuhuda wenye nguvu, na wenye uendelevu. Yanakuwa wahanga wa viongozi wenye vipawa lakini hawana

tabia njema. Wanakosa mafunzo ya kuwaendeleza kiuongozi. Hivyo wanahitaji huduma ya mafunzo mahali pao.

Wakati mwingine kanisa linaanzishwa na mishenari kutoka nchi nyingine kwa malengo kuwa baadaye litakuwa la wenyeji. Malengo ya komavu wake hupimwa kwa uwezo wa kujitegemea kwake na uwajibikaji wa viongozi wake.

Mafunzo katika ngazi ya kanisa la mahali ni lazima kwa ajili ya kuendeleza viongozi wa hapo ambao ndio hufundisha itikadi, hutumia imani ya vitendo katika maisha, na kuendeleza namna nzuri ya huduma njema na mbinu njema.

**Kupanda Makanisa**

Ni huzuni kuwa makanisa mengi hufanya kazi miaka mingi bila kupeleka injili katika jamii zingine. Makanisa yanapaswa kufunza na kutuma timu za wainjilisti kwenye maeneo ambayo hayana makanisa. Shabaha ya timu hizo ni kuwa na kundi jipya la watu waliokoka na wanakuwa kanisa.

Wainjilisti baadhi wanapaswa kufunzwa kusaidia makundi hayo ya waliokoka ili wawe kanisa. Wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwafanya waamini hawa wapya kuwa wafuasi kwa kuwafunza jinsi ya kuishi maisha ya kikrsito. Wanapaswa pia kuwa na uwezo wa kufunza kueneza injili na kuwajibika kufanya huduma.

Makanisa mengi mapya yataongozwa na mtu mwenyeji, sio na Mchungaji anayetoka kwingine na kuishi katika jamii hio. Wachungaji wengi wenye elimu kubwa hawako tayari kuchunga kanisa jipya au kutumika vijijini au miji midogo. Lazima tupate huduma ya mafunzo kwa mshirika wa mahali kanisa lipo ambaye ameitwa na Mungu kuongoza kusanyiko hilo.

**Kutayarisha Wamishenari**

Mishenari ni mtu ambaye anatumwa na kansia kwenda mahali pengine kwa kusudi la kueneza injili. Neno *mishenari* linatumika hususani kwa mtu ambaye anakwenda katika nchi nyingine na/au jamii ya utamaduni tofauti, lakini wakati mwingine linarejelea kwa mtu ambaye anaenda kwenye jamii nyingine katika nchi yake mwenyewe.

Injili inaenea haraka katika baadhi ya maeneo ya dunia, mengi ya hayo ni yale ambayo wamishenari wenyeji wanaenda kwenye maeneo mengine ya nchi zao. Hivyo mafunzo yangeongeza ufanisi wao na uimara wa itikadi zao.

Dirisha la 10/40 ni eneo la nyuzi 10 kusini mpaka nyuzi 40 kaskazini mwa ikweta, likianzia Africa kaskazini na Asia ya kusini, linajumuisha nchi za China na India. Eneo hili lina jumla ya 2/3 ya idadi ya watu duniani. Zaidi ya 80% ya watu katika dirisha 10/40 hawajafikiwa na na injili.

Baadhi za nchi za dunia hazijafikiwa na injili kwa kiwango cha kutosha ingawa miji yake mikubwa imeshakuwa na makanisa kwa miaka mingi. Mtu anaweza kutumika katika kanisa

kwa miaka mingi lakini bado hajui jinsi ya kuanzisha huduma katika eneo jipya. Anajua tu jinsi ya hubiri katika kundi la waamini walioko katika jengo la kansia. Kanisa linapaswa kufunza wamishenari kupeleka ujumbe wakiwa na shabaha ya kuanzisha familia ya waamini katika jamii hiyo.

# Sura ya 2
# Utangulizi wa Shepherds Global Classroom

## Maono ya Shepherds Global Classroom

Maono ya SGC ni kutayarisha mwili wa Kristo kwa kufanya mafunzo ya huduma ya wenyeji kuwepo ulimwenguni kote.

Kampuni moja ya taksi iitwayo Uber husafirisha abiria wapatao milionio 5.5 kila siku. Hili linahitaji nguvu kazi kubwa ya madreva wenye magari. Uber hainunui maelfu ya magari; badala yake, wanakodisha madreva wenyeji kutumia magari yao wenyewe kubeba abiria wa Ubar. Wanatatua tatizo la kazi kwa kufanya biashara hiyo. Hivyo hivyo SGC inafanya mafunzo kupatikana kila mahali kwa kuwatayarisha waalimu wenye uwezo ambao tayari wapo mahali pale. Mungu amewapa waamini karama, uwezo na hamu ya kufundisha.

## Msingi wa Itikadi

SGC haihusiani na dhehebu fulani. Tunaamini katika itikadi ya Utatu wa kihistoria kama inavyoelezwa katika kanuni ya imani ya Nisea, Kalsedonia na Athanasia. Tunaheshimu kuwa Biblia ina mamlaka yote. Tunafuata itikadi ya kievangeliko ya neema, imani, na wokovu. Tunaamini kwamba kazi ya neema ya Mungu kwa mwamini humfanya kuwa na moyo mtakatifu na kuishi maisha ya ushindi.

## Mpango wa Somo Wenye Kusudi

Walimu watarajiwa walioko kati ya wenyeji wanahitaji mtaala maalumu ambao utawatayarisha kutoa huduma ya mafunzo. Mtaala wa SGC umetayarishwa kipekee:

- Unagusa kikamilifu itikadi ya ki-evangelical katika masomo 20
- Umetayarishwa na wakufunzi mahiri, wenye uzoefu, na wenye uelewa wa tamaduni tofauti.
- Unafaa kwa kila tamaduni.
- Umeandikwa kwa lugha rahisi na unaeleweka.
- Unakazia ukweli wa kiinjili bila kuonyesha tofauti ya kimadhehebu.
- Ni wa kivitendo na unafaa katika maisha na huduma
- Unaweza kubadilika kulingana na mazingira na aina tofauti za makundi.
- Unapatikana katika lugha nyingi.
- Unatumia vipawa ambavyo Mungu ameviweka katika kanisa la wenyeji.

- Unatayarisha viongozi kuwa wakufunzi ambao wana imarisha mafunzo katika kanisa la wenyeji.
- Unatayarisha kwa haraka washiriki kufunza wengine.
- Umetayarishwa kujifunzia katika kundi lakini pia unafaa kujifunza kwa mtu binafsi.
- Unapatikana bure katika muundo wa nakala laini.
- Hauhitaji vitabu vingine vya rejea.



Waandishi wa masomo wamepata mafunzo katika elimu ya juu, wana uzoefu katika mafunzo, na kufanya huduma kati ya tamaduni tofauti.

Masomo ya SGC yana mambo ya msingi kuhusu mafunzo ya kufanya huduma. Yanafaa kwa kufundishia makundi mbalimbali, kama vile darasa la wachungaji au kundi la kujifunzia Biblia nyumbani.

Masomo yamepangiliwa ili kuharakisha utayarishaji walimu wenyeji kuendesha mafunzo. Mtu mwenye ukomavu wa kiroho, maarifa ya Biblia, na karama ya kufundisha anaweza kufundisha masomo haya hata kama hajawahi kupata mafunzo mengine.

Masomo yamepangiliwa kuwa rahisi kufundisha, yakiwa na maswali ya mjadala na mazoezi. Kuana sehemu ambazo washiriki wanaweza kufanya mazoezi ya kufundisha kwa vitendo. Urefu wa kila somo ni kurasa 160, zilizogawanywa katika masomo 7-19.

Mtaala wa SGC ni kasha la vitendea kazi vya thamani kwa ajili ya kutimiza umisheni wa kanisa.

Angalizo: Ni bora washiriki wawe na maarifa ya Biblia na ukomavu wa kiroho. Masomo haya hayakupangiliwa kwa ajili ya kufanya waamini wapya kuwa wafuasi. Tunapendekeza kutumia *Cultivate Discipleship Lessons* (ambayo pia yanapatikana kutoka SGC) kwa ajili ya wafuasi.

**Muundo wa Uhusiano wa Huduma**

Washirika wenye **mashirika ya umisheni/huduma za kitaifa** Pamoja na **Shepherds Global Classroom** watahakikisha kuwa mafunzo ya wenyeji yanapatikana. Kila shirika la kimisheni/huduma za kitaifa zitatumikia makanisa kwa kuwasaidia kuanzisha taaasisi za wenyeji.

Orodha ifuatayo inaelezea majukumu na wajibu wa

1. Shepherds Global Classroom
2. Shirika la kimisheni/huduma kitaifa, na
3. Taasisi ya wenyeji

Wanaposhirikiana kwa mafunzo ya Huduma za kikristo.

**Jukumu la Shepherds Global Classroom**

- Kutoa masomo 20 ya huduma ya mafunzo.
- Kuhakikisha kuwa masomo ya kupakua katika tovuti ya SGC yanapatikana.
- Kutoa apps zenye masomo, video, na vifaa vya kufundishia.
- Kusimamia kutafsiri masomo katika lugha mbalimbali.
- Kutoa semina ya walimu wa mafunzo na kutuma wakufunzi kwenye matukio ya kikanda.
- Kutoa vyeti kwa wahitimu.

**Jukumu la Shirika la Misheni/Huduma ya kitaifa**

- Kutoa fursa kwa makanisa kuendesha taasisi za wenyeji.
- Kuwajulisha watu kuhusu mafunzo ya SGC na fundisha walimu wa taasisi za wenyeji.
- Washirika na SGC kutoa matukio ya mafunzo ya kikanda.
- Kupanga kuchapa na kusambaza masomo.
- Kushauri kutumia tovuti ya SGC na app za vifaa vya mafunzo.
- Kuwasiliana na walimu mara kwa mara ili kutoa ushauri na vifaa vipya.
- Kuhakiki masomo yaliyosomwa tayari kwa minajili ya kutoa vyeti.

**Majukumu ya Taasisi ya wenyeji**

- Kutoa mahali pa madarasa kukutania.
- Kuchagua walimu wenyeji na kuwapa msaada kama itahitajika.
- Kuandikisha na kufunza washiriki.
- Kulipia gharama za uchapishaji wa masomo.
- Kupanga ratiba na kuendesha mafunzo.

Sura ya 8 inaelezea kwa kina uhusiano kati ya shirika la kimisheni/huduma ya kitaifa na taasisi ya wenyeji.

# Sura ya 3
# Sifa ya Mwalimu Mtarajiwa

## Huduma Maalumu

Walimu ni watu maalumu. Mtume Yakobo anatuonya kwamba sio kila mtu anaweza kuwa mwalimu, kwa sababu walimu wana uwajibikaji wa ki-pekee mbele ya Mungu na watahukumiwa ikiwa hawatakuwa waaminifu (Yakobo 3:1).

Mtume Paulo anaonya kwamba mtu anaweza kujivunia maarifa na kudharau wengine (1 Wakorintho 8:1). Alisema upendo hutusukuma kuwajenga wengine na sio kujiinua wenyewe. Watu wenye maarifa wanapaswa kutambua kuwa maarifa hayo ni zana kwa ajili ya kusaidia wengine na wala sio kitu cha kuwafanya wajione bora. Kama wanatafuta heshima kupitia maarifa, watakuwa na msukumo mbaya na watasababisha madhara.

Maonyo hay ani muhimu kwa watu wanaotaka kufundisha au kutumika katika jukumu lolote la huduma, kwa sababu wanapaswa kusukumwa kujifunza ili kutumika pamoja na maarifa yao.

## Mabadiliko ya Kweli

Kujifunza Biblia kunahitaji dhamira ya dhati ya wanafunzi. Watu wanaweza kujifunza sayansi au hesabu bila kuona matumizi yake katika tabia zao. Wanafunzi wanaweza kutobadilika kwa maarifa wanayopata. Ukweli wa kibiblia ni tofauti. Wanafunzi wa Biblia hujiona tabia zao zinabadilika wanaposoma. Wanapaswa kumruhusu Roho Mtakatifu kwa unyenyekevu kuwabadilisha tabia zao ili kuendana na kweli wanazojifunza. Kweli za kibiblia zinaleta mabadiliko.

## Sifa za Mwalimu wa SGC

Kwa nyongeza ya tabia zilizoelezewa katika sura hii, mwanafunzi wa somo la kufunza mwalimu anapaswa kuwa mshiriki wa kanisa la mahali na amependekezwa na mchungaji.

Mwalimu wa SGC anapaswa kuwa mkomavu kiroho, mwenye stadi za kufundisha, na mwenye maarifa ya kibiblia.

Matakwa ya kitaaluma: Mwalimu anapaswa kuwa na uwezo wa kusoma, kuelewa na kuelezea dondoo za somo kwa ufasaha. Ingawa mwenye cheti cha shahada anaweza kumtayarisha mwalimu kwa mbinu na maarifa ya kina, lakini maono ya SGC ni kuendeleza walimu wanaoweza kuhamishia mafunzo hayo kwa wengine. Kwa sababu hii, hatukusudii kutafuta walimu wenye vyeti vya shahada. Tunamtegemea Mungu kwa uaminifu wake atatoa karama za kiroho kwa walimu watarajiwa kila mahali. Tunatarajia kupata na kutayarisha watu ambao wamepewa karama na uwezo wa kufundisha.

Orodha inayofuata hapa chini inajumuisha tabia zingine ambazo ni muhimu pia. Mwalimu sio lazima awe ana sifa hizi zote lakini anapaswa kujiboresha katika zote. Mwalimu anayepungukiwa sifa yeyote kati ya hizi ufanisi wake utakuwa mdogo.

1. **Ukomavu wa kiroho**. Mwalimu anapaswa kuwa mfano mzuri wa tabia za kiroho. Kama maisha ya walimu wa kikristo na mitazamo yake hazilingani, hawatakuwa mfano mzuri kwa washiriki.

2. **Kupatikana**. Kama ratiba ya mwalimu imejaa tayari na hawezi kuifuata vizuri, atakuwa hapatikani kwa huduma ya kufundisha katika vipindi vyake. Kufundisha kunatakiwa kuwa kipaumbele cha mwalimu. Baadhi ya watu wenye vipawa hawapaswi kupewa huduma hii endapo wanashughuli nyingi kiasi cha kutofanya vizuri kwa kuingiliwa na shughuli zingine.

3. **Kutegemewa**. Walimu ni lazima wawe ni watu ambao wanatimiza majukumu yao. Wanapaswa kwenda na muda na kufuata ratiba. Washiriki watakatishwa tamaa kama walimu hawaji au wanakuja darasani kwa kuchelewa.

4. **Kujiamini**. Ni lazima walimu waamini kwamba wanaweza kujifunza jinsi ya kuongoza kikundi. Wanaweza kuhitaji usimamizi kwa vitendo ili kuwajengea kujiamini.

5. **Uwezo wa kutatua matatizo**. Walimu wanahitaji kuwa na uwezo wa kutunza mitazamo sahihi endapo watu hawataelewana na wanasababisha matatizo. Wanahitaji kusimama katikati ili kusaidia kutatua mgogoro huo.

6. **Uwezo wa kufundisha**. Je, watu wanaelewa ufafanuzi wa mwalimu? Mwalimu anapaswa asiwe mtu anayechanganya washiriki.

7. **Njaa ya Neno la Mungu**. Walimu wanapaswa kuwa watu wanaolifurahia Neno la Mungu, ili wawaalike wengine kuja kulifurahi pia. Ni lazima waifanye Biblia kuwa ni muhimu katika mahusiano yao na Mungu.

8. **Kumtegemea Mungu**. Walimu lazima wafahamu kuwa matokeo ya kiroho yanaweza kutokea tu kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Ni lazima wawe tayari kushirikiana na Roho Mtakatifu. Ni lazima kutegemea upako kutoka kwa Mungu. Hawapaswi kujiamini kuwa ufafanuzi wao utaleta matokeo mazuri kwa sababu ya uwezo wao pake yake.

9. **Kuwa tayari kutumika**. Walimu hawapaswi kuwa watu wanaotaka kutumikiwa. Hawapaswi kutafuta huduma kwa kusudi la kuzionyesha talanta zao. Wanatakiwa kuwa jibu la mahitaji na utayari wa kujitolea.

10. **Chini ya mamlaka ya kiroho.** Walimu wanapaswa kuwajibika kiroho kwa watu wengine. Wanapaswa kufuata maelekezo ya viongozi wa kiroho.

11. **Mwaminifu katika kanisa**. Walimu wanapaswa kuwa washirika waaminfu wa kanisa mahali alipo. Mafundisho yao yanapaswa kusababisha watu kulithamini kanisa na kuwafanya wawajibike kanisani.

12. **Shauku ya kutaka kufanikiwa**. Kama walimu wana shauku ya kutaka kufanikiwa, hawatakata tamaa upesi. Watazoea mazingira ya kazi hiyo. Watatafuta taarifa za kuwasaidia kuwa na ufanisi zaidi. Kukitokea tatizo au fursa watachukua hatua stahiki. Watakuwa na nguvu na shauku.

13. **Itikadi sahihi**. Kila mwalimu anapaswa awe na msingi mzuri wa kibiblia, kievanjeliko.

14. **Uzoefu katika huduma**. Walimu wanapaswa kuwa watu ambao wamekuwa waaminifu katika huduma ya kanisa kwa muda wa kutosha.

# Sura ya 4
# Kuwaelewa Washiriki Wetu

## Sifa za kidini

Kwa kuwa masomo ya SGC yana makusudi ya mafunzo ya huduma, washiriki wanapaswa kuwa waamini wa kikristo walio na ushuhuda mzuri na maisha yanayoheshimika. Asiyeamini hataelewa au hatayathamini yale yaliyoko katika masomo.

Washiriki wanapaswa kuamini misingi ya imani ya kikristo katika ukristo wa asili, ikijumuisha itikadi ya kievangeliko. Masomo yamepangiliwa kutumikia mwili wa Kristo kila mahali, hivyo imani za kimadhehebu hazihitajiki.


Mshiriki anapaswa kuwa mshirika wa kanisa ambaye hushiriki katika ibada na ushirika wa kanisa lake. Washiriki ambao hawako tayari kuheshimu makanisa yao hawatakuwa wajumbe wazuri wa mafunzo. Wanatakiwa kuwa sehemu ya makanisa ambayo yatawaruhusu kuyatendea kazi yale wanayojifunza. Baadhi ya mazoezi yatahusisha ushirikishaji wa waamini wengine.

## Kiwango Kinachohitajika cha Kielimu

Taasisi ya wenyeji inapaswa kutumikia washiriki ambao wanaweza kusoman na kuandika vizuri. Sio lazima wawe wahitimu wa masomo ya shule, lakini lazima wajue kusoma na kuandika ili waelewe masomo na kumaliza mazoezi wanayopewa. Taasisi inapaswa kutoa cheti kwa washiriki ambao wanaweza kusoma katika kiwango hiki.

Viwango vingine vya mafunzo vinaweza kutolewa kwa washiriki ambao wanataka kujifunza lakini hawana uwezo wa kufanya mazoezi wanayopewa. Kwa mfano, walimu wanaweza kufundisha kusanyiko kubwa au kikundi cha kujifunza Biblia kukiwa na watu ambao hawajui kusoma vizuri na hawawezi kufanya mazoezi wanayopewa.

## Kuwaelewa Washiriki Wetu



Washiriki ambao wanaandikishwa katika SGC wako tofauti na wanafunzi wa aina za taasisi zingine. Hawa sio sawa na watoto wa shule. Wako tofauti na wanafunzi wa vyuo vikuu na tofauti na wanafunzi wengi wa vuuo vya Biblia. Walimu wanalazimika kubadili mbinu za kufundisha katika aina ya darasa la namna hii. Uwezo wa kielimu wa baadhi ya washiriki utakuwa mdogo kuliko uwezo wa mwanafunzi wa chuo. Walimu ni lazima warekebishe matazamio yao. Wanapaswa kufafanua ni namna gani washiriki wanatakiwa kufanya mazoezi yao.

Wanapaswa kukemea uvivu na uzembe, lakini uchambuzi wao kwenye mazoezi ya washiriki unapaswa kuwa wa kujenga, kutia moyo, na usioonyesha dharau.

Kumbuka, kama Mungu amewaita watu katika huduma, Mungu ndiye anawapa uwezo wanaouhitaji. Washiriki wanaweza kuwa wameshaonyesha upako na baraka za Mungu katika huduma zao. Ni wajibu wetu kuwasaidia kuwakuza. Itakuwa ni makosa kuwakatisha tamaa.

Kutakuwa na tofauti ya miaka kati ya makundi ya washiriki wa SGC. Baadhi yao wanaweza kuwa wamemaliza shule karibuni. Wengine wanaweza kuwa na umri wa kutosha kuwa babu. Labda wengine wamekuwa wachungaji kwa miaka mingi. Wakati mwingine mshiriki anaweza kuwa na umri mkubwa kuliko mwalimu.

Mshiriki mwenye umri wa miaka ishirini aliyemaliza shule anaweza kuwa na uwezo mkubwa wa kitaaluma kuliko mchungaji ambaye ana umri wa miaka sitini. Hata hivyo, kila mtu anapaswa kupewa heshima. Tunapaswa kutoheshimu uwezo wa kielimu kwa namna ambayo inawakosea adabu wenye ukomavu na uzoefu. Tukiwa tunasisitiza matakwa ya kielimu, tunapaswa kuepuka kuwaibisha washiriki ambao hawajapitia mafunzo kama hayo.

## Tabia za Watu wazima wanaojifunza

Neno hili la *mwanafunzi mtu mzima* hutumika kumwelezea mshiriki ambaye ameshaanza maisha ya utu uzima. Watu wazima wanaojifunza wanaweza kuwa wameoa au kuolewa na wana Watoto. Wanaweza kuwa wanafanya kazi za kulipwa au huduma. Tayari hawa wana uzoefu tofauti tofauti. Pale ambapo mtu mzima anachagua kuwa mwanafunzi tena, wanakuwa wanataka kufikia malengo fulani.

Mtindo wa mwalimu na darasa vinapaswa kuwekwa kwa namna ambayo watu wazima wajifunzao wanahitaji.

1. **Watu wazima wanaojifunza wanataka mafunzo ambayo yatawasaidia haraka.** Wanataka kujadiliana jinsi ya kufanya kwa vitendo yale ambayo wanajifunza. Darasa linapaswa kuwapa washiriki muda wa kuelezea jinsi wanavyotarajia kutumia maarifa hayo. Mwalimu hapaswi kutumia muda wote wa darasa kwa kuwasilisha mada bila kujadiliana na washiriki.

2. **Watu wazima wanaojifunza wanataka heshima.** Tayari wana majukumu ya utu uzima na hawataki kufanyiwa kama watoto. Walimu wanapaswa kuwa na mtazamo wa kujifunza kupitia wengine na kuwa tayari kupokea jambo jipya tofauti na lao. Wanapaswa kuonyesha heshima kwa uzoefu na maarifa ya washiriki wao.

3. **Watu wazima wanaojifunza wanataka kufanya chaguzi wanaposoma.** Uzoefu wao na malengo yao vinafanya aina fulani ya kujifunza inayowavutia na inayowafaa wao. Wanahitaji uhuru kufuata matarajio yao na kuendeleza mtindo wao wa kujifunza.

4. **Watu wazima wanaojifunza hutaka kufanya mazoezi ya vitendo darasani.** Mwalimu anapaswa kuwafanya washiriki kuwasilisha mijadala yao darasani, wakielezea sehemu ya mada, na kuwasaidia kujibu maswali. Wakati mwingine washiriki wanaweza kusimulia visa walivyokutana navyo katika uzoefu wao wa maisha. Ingawa walimu ni lazima waepuke kupoteza muda, wanapaswa vilevile kufahamu kwamba simulizi inaweza kuwa njia ya mshiriki kutumia katika Maisha yake kitu alichojifunza.

5. **Watu wazima wanaojifunza wanajenga mahusiano na washiriki wenzao.** Hujifunza kutokana na mirejesho ya wenzao. Hutoa na kupokea heshima. Watu wazima wanaojifunza watakumbuka na kuthamini maishani mambo kadhaa waliyojadiliana. Darasa kwa nyakati tofauti linahitaji kugawanyika katika vikundi vidogo ili wafanye mijadala.

6. **Watu wazima wanaojifunza hutaka kukata shauri**. Wanategemea maoni tofauti kuvumiliwa.

7. **Watu wazima wanaojifunza wanataka kumpenda na kumheshimu mwalimu.** Hawategemei kuona hadhi tofauti kati yao na mwalimu kama vile tofauti ilivyo kati ya wanafunzi na profesa katika vyuo vikuu. Wanathamini kusikilizwa binafsi na mwalimu. Wanatamani sio maarifa tu lakini pia na uwajibikaji na tabia ya mwalimu.

## Mrejesho kwa Mshiriki

Mwalimu anapaswa kupata muda wa kutosha darasani na kwa mshiriki mmoja mmoja kuzungumzia mazoea mazuri ya kusoma. Washiriki wanapaswa kujifunza jinsi ya kujidhibiti na kufuata ratiba ya kusoma kila siku.

Mwalimu anapaswa kutunza kumbukumbu za mazoezi na mahudhurio ya washiriki vizuri. Mwishoni mwa somo, kumbukumbu hizo zitatumika kwa kutoa alama za somo. Wakati wa somo, ambapo washiriki binafsi hawafanyi vizuri, mwalimu anapaswa kuzungumza nao na kuwaeleza jinsi ya kuboresha.

Ni muhimu kwa mwalimu kuhakikisha mwanafunzi anaelewa jinsi ya kufanya mazoezi. Mazoezi yafanywayo vibaya yanapaswa kurudishwa kwa mshiriki ili kufanya masahihisho, lakini mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba mshiriki anaelewa jinsi ya kusahihisha kazi yake.

Kama mahudhurio ya washiriki au mazoezi yao yanafanya alama za somo kuwa chini, mwalimu anapaswa kuzungumza nao kuhusu hitaji la kuboresha. Kwa hali hiyo washiriki hawatashangazwa na alama za matokeo yao mwishoni mwa somo.

# Sura ya 5
# Mbinu za Ufundishaji Mzuri

## Mtindo wa kukaa Darasani

Mwanzoni mwa mafunzo, kuna msisimuko na matarajio. Washiriki hawajui vizuri ni nini cha kutarajia, lakini wana matumaini ya kupata msaada kutoka kwenye kikundi.

Kipindi cha kwanza kinaweza kuwa tofauti na vipindi vingine kwa sababu utatoa utangulizi na ufafanuzi kuhusu darasa ambavyo ni vya lazima. Walakini, kipindi cha kwanza kitaweka mtindo wa vipindi vingine vya baadaye. Kwa mfano, kama mshiriki fulani hatazungumza katika kipindi cha kwanza, mshiriki huyo atatarajia kuwa kimya baadaye. Kama mshiriki mwingine atakuwa anatawala mjadala, kundi litatarajia mijadala ijayo kutawaliwa na mtu yule yule. Kama darasa litakuwa shaghalabaghala, watatarajia hivyo hivyo katika vipindi vingine. Kama darasa lina ushirikishwaji mdogo wa washiriki, watatarajia mfano ule ule.

Baadhi ya washiriki wanaweza kuacha baada ya muda kwa sababu darasa halijawa kama walivyo tarajia. Darasa haliwezi kupangwa kumpendeza kila mtu, lakini linapaswa kuwa lenye kuwaridhisha washiriki wanaotaka kujifunza. Ni muhimu kuliongoza darasa vizuri ili wanafunzi wanaotarajia mambo mazuri wasikate tamaa.

## Shabaha ya Matokeo

Zao la mafunzo yetu linapaswa liwe ni ufanisi wa huduma na maisha endelevu ya kikristo. Wachungaji wenye ufanisi, walimu, wainjilisti, na wamishonari ni matokeo ya mwisho tunayoyataka kutokana mafunzo haya.

Walimu lazima waangalie matokeo ya haraka na yanayoonekana, ili kujua kama madarasa yao yanakuwa na mafanikio. Wanapaswa kujua kama madarasa yao yana fanikiwa bila kusubiri kuja kuona washiriki wanafanya vizuri katika huduma zao mbeleni.

Matokeo ya kwanza ni umakini katika darasa ambao mwalimu anapaswa kuwa nayo. Walimu lazima wadumishe utaratibu ili washiriki waweza kuwa makini. Walimu hawawezi kuwalaumu tu washiriki endapo umakini wao ni duni. Walimu lazima walifanye darasa kuwa na mvuto.

Kuna viashiria vingine vinavyoonesha kuwa darasa lina fanya vizuri. Viashiria hivi ni pamoja na ushiriki wa washiriki katika mijadala, maswali mazuri kutoka kwa wanafunzi, mahudhurio mazuri, kukamilisha mazoezi, na hamasa ya washiriki kuhusu kile wanachojifunza. Kama walimu hawataona hivi viashiria, wanapaswa kutafuta njia za kuboresha mbinu za madarasa yao.

**Malelekezo Mengine zaidi ya ufundishaji Mzuri**



1. **Thamani ya muda.** Anza na maliza darasa kwa wakati. Usisubiri kila mtu afike. Kama utaanza kwa kuchelewa utakuwa unapoteza muda wa watu waliokuja kwa wakati. Unapomaliza kwa kuchelewa unaingilia majukumu ya washiriki. Katika tamaduni zingine, kujali wakati sio jambo rahisi. Lakini watu wale wale katika tamaduni hizo wanajua kutunza ratiba kwenye kazi za ajira zao au wanaposafiri. Wanapaswa kuweka uzito wa namna hiyo kwenye darasa.
2. **Waketishe washiriki katika mkao wa nusu duara.** Ni kwakuwa mjadala ni muhiu, ukaaji unapaswa kupangwa vizuri ili washiriki waweze kutazamana.
3. **Lisiliza vizuri wanafunzi wanapoongea.** Viashiria vizuri vya kusikilizana ni kutazamana, kuwa makini katika lugha za mwili, kupuza vitu vinavyofanya akili yako kutanga tanga, na mwitikio kwenye ucheshi wa mzungumzaji au hisia zingine.
4. **Hakikisha hakuna mwanafunzi ambaye wakati wote yuko kimya.** Elekeza swali kwa mshiriki ambaye huwa hasemi sana ("Daudi, unafikiri nini kuhusu hilo?").
5. **Uliza swali ambalo washiriki wanaweza kujibu ili kujenga kujiamini.** Kama moja anatoa jibu lisilo sahihi, jaribu kuonesha kitu kizuri katika jibu lake kabla ya kufanya uchambuzi.
6. **Jaribu kusema kitu kizuri kwa kila maoni yanayotolewa kabla ya kufanyia uchambuzi.** Washiriki watajienga kujiamini endapo maoni yao yatasemewa vizuri.
7. **Usiruhusu mshiriki moja kuzungumza sana na kujibu maswali yote.** Unaweza kuelekeza maswali kwa washiriki fulani kimakusudi. Au unaweza kuuliza, "wengine mnasemaje?" katika mjadala, unaweza kusema "hebu tusikie kwa mtu ambaye bado hajasema kuhusu hili."

   Kama kuna washiriki bado wanaongea sana kuliko wengine, viongozi wanaweza kusema nao nje ya darasa. Kiongozi anaweza kusema kama hivi "Yeremia, wewe ni mfikiri haraka na unao uwezo wa kujibu haraka katika mijadala, lakini ninaogopa kuwa wengine hawatashiriki ikiwa tutajibu kila kitu haraka. Je, unaweza kunisaidia kuwapa wengine nafasi ya kushiriki?"
8. **Usiruhusu washiriki wawili au watatu kuendelea kubishana huku ukisahau wengine walioko kwenye kundi.** Kama kuna mtu anataka kuendelea kubishana kwa muda mrefu kuhusu suala Fulani, mwambie kwamba mjadala utamaliziwa baadaye.

9. **Usiruhusu yeyote kuingilia kati au kukatisha wengine.** Inua mkono wako, kwa ujasiri msimamishe anayeingilia na mruhusu mzungumzaji wa kwanza kumalizia. Vinginevyo, wakati wote mjadala utakuwa umedhibitiwa na mwanakikundi ambaye ana tabia aina hiyo. Watu ambao wana ujasiri kidogo watajisikia kuvunjika moyo kwamba hawawezi kumaliza maneno yao.

10. **Sikiliza malalamiko.** Kila lalamiko linaweza kuwa dalili ya tatizo ambalo laweza kusahihishwa. Usipuuzie viashiria vinavyoonesha kutoridhika. Kama kuna mtu haridhiki na masomo, anaweza kuwa haelewi kusudi, au anaweza kuwa ana malalamiko ya kweli.

11. **Msahihishe mshiriki vurugaji**. Kama washiriki binafsi kwa wakati wote wanaonyesha upinzani, vurugu, ubishi, au uchovu, wanaweza kuwa hawakubaliani na masomo. Wanaweza kuwa hawakutazamia darasa la namna hiyo. Zungumza nao pembeni kuwasaidia kuona kusudio la masomo.

12. **Kama hujui jibu la swali usijifanye unajua**. Mwalimu sio lazima kujua kila kitu. Itakuwa ni sawa ukimwambia mshiriki kuwa utaenda kutafuta jibu.

13. **Usiruhusu mijadala iwe fitina au uchochezi.** Usiruhusu kikundi kiwe jukwaa la kukosoa kanisa na viongozi. Wachungaji wengi wanaogopa wakati washirika wao wakijiunga na masomo.

14. **Wajue washiriki wako.** Unaweza kufundisha kwa ufanisi zaidi endapo unajua mazingira yao ya kifamilia, uzoefu wa kihuduma, elimu zao, huduma ya sasa, na malengo ya baadaye. Jaribu kujifunza mambo haya katika mazungumzo ya binafsi.

Maelekezo mengine ya ufundishaji mzuri na tabia za kujifunza kwa watu wazima zipo katika sura ya 6.

# Sura ya 6
# Jinsi ya Kufundisha Masomo ya SGC

## Darasa

Mwalimu anapaswa kupanga darasa mapema kama inawezekana. Washiriki wanapaswa kukaa kwa kutazamana. Mwalimu anapaswa kuhakikisha kwamba kuna nafasi ya kutosha na kuna hakuna vitu ambavyo vitaondoa usikivu na makelele wakati wa somo. Mwalimu anapaswa kujitahidi kuhakikisha kuwa kutakuwa na mkao wa kuridhisha, hewa ya kuridhisha na mwanga wa kutosha. Kusomea nje kunaweza kuwa kuzuri endapo hakuna shughuli za kuharibu usikivu.

Darasa linapaswa kuwa na ubao mkubwa wa kuandikia na kuchorea.

## Siku ya Kwanza ya Darasa

Walimu wanapaswa kujitambulisha, wakielezea kuhusu familia zao, uzoefu wa kihuduma, na historia ya elimu zao. Wanapaswa kuepuka kuorodhesha waliyowahi kufanya kana kwamba wanataka kuonyesha kuwa ni watu waheshimiwa. Wanapaswa kukumbuka kwamba kusudi la kuelezea habari hizi ni kujenga uhusiano na washiriki.

Washiriki wanapaswa kujitambulisha kwa ufupi. Mwalimu anaweza kuongea nao kila mmoja, akiwauliza maswali mmoja au wawili ili kuonesha kuwa anavutiwa na ana jenga uhusiano kati yao.

Baada ya kujitambulisha kunaweza kufuata muda wa maombi. Omba ili Mungu alitumie darasa kukutana na mahitaji ya wanafunzi. Mwalimu anapaswa kuonesha kuwa anamtegemea Mungu kuyafanya mafundisho kufaa na yenye kubadili maisha. Vipindi vya baadaye vya darasa vinapaswa kuanza na maombi na kwa kushirikishana mahitaji kwa ufupi.

Walimu wanapaswa kuwambia washiriki walete vifaa vya aina gani, ikiwa pamoja na Biblia, nakala ya somo lililochapwa na daftari la kuandikia. Walimu wasisitize kuwa washiriki waandike kumbukumbu kwa kuandika ili ziwe faida zao baadaye, sio kwa lengo la majaribio. (Majaribio yote yatatokana na mazoezi yaliyomo katika kitabu cha somo.)

Baada ya utambulisho, muda wa darasa siku ya kwanza unapaswa uwe ndio mfano wa madarasa yanayofuata, ili washiriki wajue wanachotarajia.

## Muundo wa Somo

Masomo ya SGC sio tu ni vitini; ni masomo yaliyopangwa kufundishia. Kila somo lina mwongozo wa mwlimu karibu na mwanzoni mwa kitabu. Masomo yanafanana na mengine lakini hayafanani katika muundo.



Masomo mengine yameanza na malengo ya somo. Sio lazima kwa mwalimu kusoma hayo katika darasa.

Masomo mengi yanaanza na swali au simulizi au na mbinu nyingine ya kuvutia na kuwafanya washiriki waone kuwa mada ni muhimu.

Walimu wanaweza kupitia ukurasa kwa ukurasa kwa somo lote, wakielezea habari za aya. Wanapaswa kujitayarisha mapema kwa kuhakikisha wanaelewa taarifa na wanapigia mistari vifungu muhimu ili kuwasaidia kuelezea kila aya.

Maswali ya mijadala yapo katika kitabu chote. Wakati mwingine swali linatambulisha taarifa inayofuata. Wakati mwingine, swali linamuuliza mshiriki kusema kitu kutokana na alichojifunza. Maswali hayahitaji majibu ya "ndio" au "hapana", bali ni kwa ajili ya ufafanuzi. Mwalimu aruhusu washiriki kadhaa kusema. Sio lazima mjadala kupata jibu la kuhitimisha kila wakati, hasa pale ambapo swali linatambulisha taarifa inayofuata.

Walimu wanahitaji kuwa na maswali yao ya ziada ili kujadili. Wakati wote walimu wanatambue kuwa wamekuwa wakiongea kwa dakika kadhaa bila mrejesho kutoka kwa washiriki, wanapaswa kuwauliza washiriki swali.

Wakati wote huwa changamoto kufanya mijadala isiwe ya kupoteza muda. Walakini, watu wengi hawawezi kujifunza bila kuwa na mjadala. Washiriki huhitaji muda kufikiri na kusikiliza wengine wakisema jinsi dhana iliyoko katika somo inavyoweza kutumika katika mazingira yao na katika maisha ya kanisa.

Masomo mengi yanamalizika kwa mazoezi. Mwalimu anapaswa kuyaelezea mazoezi. Kama darasa la siku hiyo lina mada kadhaa, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa washiriki wanaelewa mazoezi yote ambayo yanatakiwa kukamilika kabla ya kipindi kingine.

## Siku zingine za darasa

Mazoezi yatawasilishwa siku za darasa baada ya siku ya kwanza. Mwalimu anapaswa kukusanya mazoezi mwanzoni mwa darasa. Baadhi ya mawasilisho ya washiriki yanaweza kuwasilishwa mwanzoni, na mengine baadaye ili kuleta utofauti wa shughuli katika siku.

Wakati kuna jaribio au kuandika kitu kutokana na kumbukumbu zao ni muhimu kuhakikisha washiriki wanakaa vizuri wanapoandika ili waepuke kutoangalia kazi za wengine.

Mbali na kazi za uwasilishaji za washiriki, mwalimu anapaswa kuuliza mara nyingi mwanafunzi kuwasilisha sehemu ya habari iliyomo katika somo. Hili linapaswa kupangwa kabla ya muda ili washiriki waweze kujitayarisha.

# Sura ya 7
# Kugundua Walimu

## Njia Tatu za Kutumia Sura hii

1. **Mwezeshaji anaweza kutumia njia zilizomo katika sura hii ili kuendeleza walimu wenyeji.** Kama kanisa mahali lilipo halina mtu anayejisikia ana uwezo wa kufundisha, mwezeshaji hawezi kuanza haraka masomo yanayojitegemea. Mwezeshaji lazima amgundue na kumwedeleza mwalimu mtarajiwa. Sura hii inamwelezea mwezeshaji jinsi ya kupata mwalimu mwenyeji.

2. **Mwezeshaji kutayarisha walimu wenyeji jinsi ya kutumia mbinu hii kwa wanafunzi wao.** Kama walimu wenyeji wa eneo jipya tayari wana uwezo wa kufundisha, mwezeshaji hahitaji kutumia zoezi katika sura hii. Mwezeshaji anapaswa kujifunza mbinu hii kwa walimu wenyeji ili waweze kutumia mazoezi ya kuwaendeleza washiriki.

3. **Mwalimu mwenyeji kuwandeleza washiriki.** Kila mwalimu anapaswa kuwa na juhudi za kuendeleza ujuzi wa huduma ya washiriki.  Mbinu zilizoelezwa katika katika sura hii zitafaa kuwasaidia washiriki kuanza kuzumza katika makundi.

## Hitaji la Kuwagundua Walimu

Mara nyingine wawakilishi wa SGC wanapotembelea makanisa wanakuta watu walio tayari kuanza kufundisha. Kwa kawaida, walimu hawa watarajiwa ni watu walio na taaluma na wana uzoefu wa kufundisha. Wanaweza kuyaangalia masomo na kuona kuwa ni rahisi kuyafundisha. Maelekezo yamechapwa mwanzoni mwa kila somo. Kuna maswali ya mjadala. Sio kwamba masomo haya ni kitabu tu; yanaweza kufundishwa kama yalivyo.

Masomo yamepangiliwa kiasi kwamba mtu mwenye ujuzi wa kusoma, uelewa wa Biblia, na uwezo wa kufundisha anaweza kujifunza haraka kuvitumia. Walakini, wakati mwingine watu ambao hawana mafunzo ya kitaaluma hujisikia kwamba hawana uwezo wa kufundisha. Wanafikiri kwamba ni watu waliopata mafunzo ya juu tu ndio wanaweza kufundisha.

Mungu amewapa watu wengi ambao hawajapata fursa ya kupitia vyuoni uwezo wa kufundisha. Ni kwa kuwa walimu ni muhimu kwa kanisa, Tunaweza kuwa na ujasiri kwamba kwa kawaida Mungu ana watu wenye uwezo wa kufundisha mahali popote ambapo kuna kanisa (Waefeso 4:11-12).

Watu wengi hawatambui kuwa tayari wamepata ujuzi wa kufundisha kwa kupitia maisha yao ya kila siku. Huwa wanaelezea mambo nyumbani na wakiwa kazini. Wanasaidia watu kutatua matatizo yao. Wanayo sifa njema kuwa wanauwezo wa kuelezea mambo.

Walipokuwa wanafunzi mashuleni walikuwa na ujuzi wa kusoma na kuelewa na kueleza. Hawajui kuwa wana uwezo wa kufundisha.

Mwezeshaji anapaswa kuwasaidia walimu watarajiwa kugundua uwezo wao kupitia uzoefu wa kuongea walionao. Kupitia uzoefu, mtu anaweza anaweza kujiamini kuzungumza katika kikundi.

## Njia za kupata Uzoefu katika kuongea

1. **Wape Zoezi la kuongelea Mada rahisi.** Hotuba iwe ya muda wa dakika chache. Kama washiriki wanajisikia aibu kusimama mbele ya kikundi wape fursa kutoa hotuba zao wakati wamekaa katika viti vyao.

   Mifano ya mada za rahisi kuzungumzia:

   - Zungumzia changamoto ulizopitia ukiwa mtoto.
   - Zungumzia kuhusu ndugu ambaye alikuwa muhimu kwako.
   - Mulize mshiriki mwingine maswali ndipo mtambulishe mshiriki huyo katika kikundi.
   - Ni mahali gani ungependa kutembelea? Kwanini?
   - Zungumzia mstari moja wa Maandiko unaoupendelea.
   - Zungumzia siku zima inavyokuwa ukiwa kazini kwako.
   - Unakumbuka nini kutokana na mahubiri uliyosikia hivi karibuni?

2. **Katika darasa mwelekezee mtu swali.** Swali liwe la kutaka maelezo, sio majibu mafupi ya ndio na hapana. Swali lihusu jambo ambalo mshiriki anaweza kujibu, ili ajiamini zaidi na sio kujisikia amedhalilishwa.

3. **Omba mshiriki moja kuelezea mazoezi yao ya kikundi waliyoandika.** Masomo yanahitaji mazoezi aina mbalimbali ya kuandika. Hata kama mwezeshaji amekuja kwa siku moja, washiriki wanaweza kupewa moja ya zoezi la kuandika na kuliwasilisha.

4. **Wagawe katika vikundi vya watu watatu kwa ajili zoezi la kufundisha.** Mpatie kila mtu sehemu fupi afundishe katika kikundi. Hii inafanya kuwa na watu wachache na kuwapatia fursa washiriki kadhaa kufanya zoezi kwa wakati moja.

5. **Omba mshiriki aelezee sehemu ya somo.** Sehemu nyingi katika somo zina aya chache zinazoelezea dhana husika. Muombe mshiriki mapema kujitayarisha kuelezea sehemu hiyo kwa dakika chache.

6. **Omba mshiriki mwenye uelewa mzuri kufundisha mada kutoka moja ya masomo.** Utaratibu rahisi kwa mshiriki ni kufundisha mada ambayo amesikia mtu

mwingine akifundisha. Mshiriki ataonesha uwezo wake wa juu anapojitayarisha na kufundisha somo ambalo hakuna aliyemfundisha. Mwezeshaji anaweza kujisikia kuendelea kufundisha zaidi kadiri inavyowezekana, na darasa likafurahia kumsikiliza mwezeshaji, lakini kumbuka lengo ni kuwatayarisha wengine kufundisha.

7. **Tumia mbinu za "meza ya duara" Washiriki.** Wanakaa wakizunguka meza wakiwa na somo lilochapwa. Hakuna mwalimu katika meza hiyo. Washiriki mbalimbali wanaachiana kuzungumza kitu kuhusu mada. Mtu moja katika meza anapewa wajibu kuongoza na kuendeleza mjadala kwa kuuliza mwitikio kutoka kwa washiriki. Kiongozi huyu sio mwalimu. Kikundi kitagundua kuwa kinafanya kazi na kujifunza bila mwalimu. Mbinu hii inawezesha kikundi kujiunda hata mahali ambapo hakuna mtu ambaye anasifa ya kufundisha.

## Hitimisho

Maono ya SGC ni kuifanya huduma ya mafunzo kuwa ya wenyeji kila mahali. Mafunzo yanaweza kuwa kila mahali kupitia watu ambao Mungu amewapa uwezo wa vipawa na uelewa wa Biblia. Wawezeshaji wanapaswa kukubuka kuwa kusudi lao sio tu kutoa maarifa lakini pia kuwatayarisha washiriki kuieleza kweli kwa wengine.

# Sura ya 8
# Kuendesha Taasisi ya Wachungaji Wenyeji

## Utangulizi

Masomo ya SGC yanatumika katika mafunzo ya namna tofauti tofauti. Shule za sekondari baadhi zinaweza kutumia baadhi ya masomo. Makanisa kadhaa yanatumia masomo haya katika shule za jumapili kwa watu wazima. Vikundi vya kujifunza Biblia manyumbani huchagua masomo haya na kujifunza. Wachungaji huchagua taarifa kutoka masomo haya na kutumia katika mahubiri na kufundisha.

Maelekezo katika sura hii yanatumika katika utendaji wa taasisi ya wenyeji ambao wanatumia masomo 20 ya SGC katika mafunzo yote.

## Kiwango cha kielimu



Masomo yote ya SGC yana masomo muhimu wa mtaala wa chuo cha Biblia. Yameandikwa bila kutumia misamiati migumu.

Mshiriki lazima awe na uwezo wa kusoma, kuandika vizuri na kujifunza masomo kama ilivyokusidiwa.

Masomo haya hayakukusudiwa kwa waongofu wapya, ingawa taarifa nyingi zinafaa kwa kusudi hilo.

Njia nzuri kwa kikundi ni kwamba kila mshiriki kuwa na:

1. Nakala ya somo
2. Kukamilisha mazoezi yote
3. Kupewa nafasi kuwasilisha taarifa katika kikundi
4. Kuwa na mahusiano mazuri na kanisa anakotoka, na
5. Awe na huduma mara nje na kikundi chake

Mwezeshaji anayedumisha vitendo hivi atakuwa anafundisha washiriki kwa ufanisi wa huduma.

Kuna machapisho ya makundi ya wanafunzi ambao hawajitayarishi kwa huduma. Machapisho haya ni muhtasari wa masomo. Yanatumiwa katika shule za sekondari na shule za jumapili za watu wazima. Wanaosoma masomo haya hawahitajiki kufanya mazoezi ya kawaida kwa kuwa hawafanyi mazoezi ya huduma au hawajitayarishi kwa kazi ya huduma. Machapisho haya hayapaswi kutumika kwa wanafunzi wanaojitayarisha na huduma na na na wenye mpango wa kupata cheti cha huduma. Wawezeshaji wa washiriki hawa lazima wafundishe kwa kufuata kitabu cha masomo ya SGC kwa kuwa machapisho hayo hayana taarifa zote.

SGC haitoi shahada ya ki-somi. Mahali pengine taasisi za wenyeji au taifa zinatumia masomo ya SGC kutoa stashahada au cheti kwa kuzingatia vigezo vyao. Mshiriki lazima aandikishwe na kituo na atimize masharti yao.

Mahali ambapo shahada ya kitaaluma haipatikani, masomo haya yatazamwe kama mafunzo ya stadi za kazi. Katika ulimwengu wa kazi mafunzo ya stadi za kazi humtayarisha mtu kufanya kazi za stadi. Masomo hayo huwa hayahitaji shahada, lakini yanamwidhinisha mtu kuwa amepata mafunzo. Hivyo hivyo, masomo ya SGC ni mafunzo ya stadi kwa huduma.

## Vifaa Vinavyohitajika

Ni Biblia tu ndiyo inayohitajika kwa ajili ya masomo, lakini masomo yenyewe yanapendekeza kusoma taarifa za ziada. Taasisi za wenyeji zinapaswa kujenga uwezo wa maktaba kwa ajili ya matumizi ya washiriki.

## Ratiba ya Darasa

Taasisi ya wenyeji inaweza kuwa na ratiba yake ya masomo, kulingana na mazingira yake. Walakini, muda wa kutosha lazima uzingatiwe. Kama mwezeshaji atafundisha bila kuwa na mjadala na mazoezi ya wanafunzi, muda utakaotumika utakuwa kidogo, lakini ufundishaji huo hautawatayarisha washiriki vizuri. Kama kikundi kitatumia muda kujadiliana taarifa na kukamilisha mazoezi, somo litachukua masaa ya darasani zaidi ya thelathini. Washiriki wanapaswa kutumia muda wa ziada kufanya mazoezi nje ya wakati wa darasa.

## Mpangilio wa Masomo

Mtiririko wa aina fulani sio wa lazima. Kila darasa linajitosheleza na halitegemei kuendeleza darasa jingine. Kuna uwezekano kuendesha darasa kwa mzunguko, likiruhusu washiriki wapya kujiunga mwanzoni mwa kila somo. Taasisi inaweza kuendelea kufunza washiriki wapya kuliko kuwafanya wangoje hadi mwanzoni mwa mwaka. Washiriki wanaweza kujiandikisha mwanzoni mwa somo lolote na kuendelea katika mzunguko wote mpaka wamemaliza masomo yote.

## Uthibiti Ubora

Mwezeshaji anapaswa kutunza taarifa za mahudhurio ya washiriki. Mshiriki asiyehudhuria ngalau 75% ya muda wa darasa na kukamilisha mazoezi yanayotakiwa kwa 100% hatapewa daraja la somo. Katika mazingira maalumu, mwezeshaji anaweza kutoa masharti ya kujifunza kwa ziada ili kulipiza muda wa darasa uliopotea.

Mwezeshaji anapaswa kutunza kumbukumbu za taarifa zilizokamilika kwa umakini ili kuhakikisha daraja la mwisho liko sahihi na la haki. Mwezeshaji lazima ahakikishe kuwa wanafunzi wanajua binafsi kama mazoezi yao au mahudhurio yao yanasababisha kushuka daraja.

Kama taasisi ya wenyeji ni sehemu ndogo ya umoja wa taasisi nyingi, kumbukumbu za taarifa za mahudhurio na mazoezi yanapaswa yawepo kwa ajili ya kukaguliwa na wakaguzi wa kanda. Cheti hakitakuwa na thamani kama taasisi haifuati matakwa muhimu.

## Fedha za Uendeshaji za wenyeji

Kila mahali ilipo taasisi ya wenyeji lazima ijitegemee. Darasa linatolewa na kanisa. Wawezeshaji wanatumika kama sehemu ya huduma ya kanisa la hapo. Gharama za kuchapa masomo itatolewa na kanisa la hapo au wanafunzi. Kama kituo ni sehemu ya umoja wa vituo vingi, uongozi mkuu unaweza kupanga ada kwa washiriki ambayo inaweza kutosheleza gharama ya kuchapa masomo na kusaidia walimu wa hapo.

Ni lazima walimu wa pale wawe waaminifu na wenye uwazi katika masuala yote ya fedha. (2 Wakorintho 8:21). Kila moja anayehusika lazima ajue fedha kiasi gani zimekusanywa na jinsi zilivyotumika. Kamati lazima ihusike katika kudhibiti fedha. Mfano wa masuala ya kifedha ni pamoja na ada wanazolipa washiriki katika taasisi au kituo cha uongozi mkuu, gharama za kuchapisha masomo, kuwapa posho wawezeshaji wa kituo, na fedha zozote zilizokusanywa au au kutumika.

Kwa kuwa uaminifu ni tabia ya msingi ya mkristo, haiwezekani kwa mtu ambaye sio mwaminifu kuwa mkristo wa mfano. Mtu ambaye siye mwaminifu hapaswi kushika nafasi ya huduma yeyote. Aina yeyote ya kutakuwa mwaminifu itaadhiri uhusiano wa kiongozi na SGC.

## Shirika la kimisheni/Huduma ya Kitaifa na taasisi ya wenyeji katika kushirikiana

ABC ni jina la kubuni la huduma ya taifa ambayo husaidia makanisa kuimarisha taasisi za wenyeji. Makubalino ya eneo inayotumia ABC kwa taasisi za wenyeji yanapatikana katika ukurasa unaofuata. Mwakilishi wa ABC hutembelea eneo la taasisi ya wenyeji mara kwa mara na kukagua akitumia orodha ya maswali yaliyopo mwishoni mwa sura hii.

## Mfano wa Makubaliano ya Eneo

*ABC hutumia fomu hii kuelezea uhusiano kati ya **huduma ya kitaifa** na **taasisi ya wenyeji.***

Kusudi la ABC ni kutumika katika mwili wa Kristo kwa kuliwezesha kanisa kuendeleza huduma ya viongozi. Kanisa la mahali au shirika la huduma linaweza kukubaliwa kuendesha huduma ya mafunzo kwa kutumia masomo ya SGC.

ABC itahifadhi haki ya kuvunja makubaliano haya endapo kanisa la mahali halitatimiza wajibu wake.

**ABC hutoa yafuatayo:**

- Vitabu 20 vya masomo ya mafunzo
- Mafunzo ya semina ya wawezeshaji
- Wasimamizi kutembelea maeneo ya mafunzo kutia moyo wawezeshaji wenyeji na kuthibiti ubora.
- Vyeti vya wanafunzi kwa kila somo waliyomaliza (nakala ya somo ya kila mtu binafsi ni lazima kwa kila mshiriki kupokea cheti)
- Cheti cha kumaliza masomo yote
- Kibao cha tangazo la ABC kitakachowekwa katika eneo la Huduma

**Huduma ya wenyeji watafanya yafuatayo:**

- Kutoa wawezeshaji mwaminifu, wenye uwezo na kuthibitishwa na uongozi wa ABC
- Kuwataka wawezeshaji kushirikiana katika mafunzo na kufuata mwongozo kutoka uongozi wa ABC
- Kutoa chumba kinachofaa kwa mafunzo
- Kuwasaidia wawezeshaji wenyeji kifedha kadiri itakavyo lazimu
- Kukusanya na kutuma kwa ABC ada ya kujiandikisha kwa kila kitabu cha somo linalohitajika
- Kupatia uongozi wa kumbukumbu za mahudhurio ya washiriki na mazoezi yao yaliyotayari.
- Kuweka kibao cha tangazo litolewalo na ABC. Kibao hicho ni mali ya ABC na kitaondolewa wakati wa kuvunja makubaliano.

Jina la Huduma ya wenyeji ___________________________________________
Saini ya mwakilishi wa Huduma ya wenyeji ______________________________________
Saini ya mwakilishi wa ABC ____________________________________

**Mfano wa maswali kwa ukaguzi wa taasisi ya wenyeji**

*Wawakilishi wa ABC wanapokuja kutembeleaeneo, watatumia maswali yafuatayo kutadhimini na kutoa mwongozo wa kuboreshaji.*

1. Je, eneo lina wawezeshaji ambao wamepokea mafunzo ya SGC?
2. Je, wawezeshaji wanatumia mbinu tofau tofauti za kufundishia?
3. Je, wawezeshaji wanawahusisha washiriki katika mjadala na kushiriki kweli?
4. Je, eneo linaendeleza wasaidizi wa mwezeshaji ambao wanafanya mazoezi ya kufundisha darasani?
5. Je, darasa linafaa kwa kujifunzia (ukaaji, mwanga, hakuna kelele na mwingiliano wa shughuli)?
6. Je, kila mwanafunzi huwa anapata nakala ya somo lolote linafunzwa?
7. Je, washiriki wote wanaweza kusoma na kuandika vizuri kiasi cha kukamilisha mazoezi? (Takwa la kupata cheti).
8. Je, ratiba ya darasa hutoa masaa thelathini kwa kila somo kwa kuongezea muda utumikao katika kukamilisha mazoezi?
9. Je, mchakato wa majaribio huhakikisha washiriki hawaangaliziani majibu au kuangalia katika makaratasi waliyoingia nayo?
10. Je, wawezeshaji wanatunza kumbukumbu sahihi za mahudhurio ya washiriki? (Mshiriki akikosa zaidi ya 25% ya masaa ya darasa hapaswi kupokea tuzo za somo.)
11. Je, wawezeshaji wanatunza kumbukumbu za mazoezi ya wanafunzi ambayo yamekamilika? (Mazoezi yote lazima yakamilishwe ili kupata cheti. Mazoezi kutoka darasa linaloendelea yanatakiwa kuwepo kwa ajili ya tathmini mpaka yatakapo rudishwa kwa washiriki mwishoni mwa somo.)
12. Je, taasisi ya wenyeji inaweka mfumo wao wa fedha za kuendeshea?
13. Je, fedha za taasisi za wenyeji zinadhibitiwa na kamati ya wenyeji katika hali ya uwazi na uwajibikaji?

# Rasilimali za SGC Mtandaoni

### App ya Shepherds Global Classroom

SGC app inapatikana katika apple store na Google play.

App ina masomo ya kujifunza au kupakua. Tafsri katika lugha mbali mbali zimekuwa zinapatikana kila moja ikikamilika.

### ShepherdsGlobal.org

Tovuti ina masomo kwa ajili ya kupakua na taarifa zingine.

### Mafunzo ya Mwezeshaji

*Kitabu cha Taasisi za Wenyeji* kinaweza kupakuliwa kama dokiment. Matoleo ya Video za mafunzo ya somo katika lugha mbali mbali zitakuwa zinaongezwa zinapokamilika.

### Uwasilishaji wa slaidi

Lugha ya Kiingereza ina slaidi za kuonyesha kwa kupakua bure.

### Video za kuhamasisha

Tovuti ina video kutoka viongozi wa SGC, wawezeshaji, na washiriki wakielezea maono na mvuto wa masomo.

### Rekodi za Sauti na Picha za video

Rekodi za sauti na video za masomo yakifundishwa zitapatikana katika lugha mbali mbali kwa kadiri kila moja ikikamilika.

# Maelezo ya Kozi za Shepherds Global Classroom

### Kuchambua Agano la Kale

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

### Kuchambua Agano Jipya

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

### Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inasoma maisha ya Yesu kama mfano kwa huduma na uongozi katika karne ya 21.

### Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na dhamira kama inavyoelezewa katika vitabu ya Warumi, kujadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa ya kutatanisha katika kanisa.

### Kanuni za Tasfiri ya Kibiblia

Kozi hii inafundisha kanuni na njia za kutafsiri Biblia vizuri ili kuongoza maisha yetu na mahusiano na Mungu.

### Imani za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea mafundisho ya Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, Mwanadamu, Kristo, Wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na Vitu vya Mwisho.

### Eskolojia

Kozi hii inafundisha vitabu vya kibiblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu zingine za maandiko ya kinabii na inasisitiza mafundisho muhimu kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa Mungu wa milele.

### Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

### Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa

Kozi hii inaelezea ubunifu na mpango wa Mungu kwa kanisa na masomo ya kibiblia kama vile uanachama wa kanisa, ubatizo, ushirika, zaka, na uongozi wa kiroho.

**Historia ya Kanisa I**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyotimiza dhamira yake na kutunza mafundisho muhimu kuanzia kipindi cha kanisa la mwanzo mpaka Matengenezo.

**Historia ya Kanisa II**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyopanuka na lilivyopitia changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo mpaka nyakati za kisasa.

**Uundaji wa Kiroho**

Katika kozi hii wanafunzi wanajifunza kuwa na mitazamo ya yesu, kuwa na Mungu kama Yesu alivyokwa na baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kufanya nidhamu ya kiroho na binafsi ya yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) lililoundwa na Yesu.

**Huduma ya Uongozi**

Kozi hii inahimiza tabia ya Kikristo wakati inafundisha viongozi kuongoza mashirika kupitia mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushirikishana maono, kuweka malengo, kupanga mkakati, kuchukua hatua, na kupitia mafanikio.

**Kanuni za Mawasiliano**

Kozi hii inafundisha theolojia ya mawasiliano, njia za kuzungumza kwa ufanisi, na njia za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

**Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi**

Kozi hii inatoa kanuni za kibiblia ambazo huongoza mbinu za uinjilisti. Inaelezea aina za uinjilisti na kutoa masomo ya kutumia kufundisha wapya waliobadilishwa.

**Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani**

Kozi hii inafundisha misingi ya kisayansi, kihistoria, na kifalsafa kwa mtazamo wa ulimwengu wa Kikristo, na inaonyesha jinsi gani imani ya Kikristo ni thabiti katika hoja na hali halisi.

**Dini za Ulimwengu na Ibada**

Kozi hii huumpa muumini wa kiinjili uelewa wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya dini.

**Utangulizi wa Kuabudu Kikristo**

Kozi hii inaelezea jinsi gani kuabudu huathiri nyanja zote za maisha ya muumini na hutoa kanuni ambazo humuongoza mtu binafsi na mkutano wote mazoezi ya kuabudu.

**Kuishi Kikristo kwa Vitendo**

Kozi hii hutumia kanuni za kiroho kwa utumiaji wa fedha, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na maeneo mengine ya kuishi kwa vitendo.

**Ndoa ya Kikristo na Familia**

Kozi hii inatoa mtazamo wa Kikristo kuhusiana na maendeleo ya binadamu kupitia hatua mbalimbali za maisha na zinatumia kanuni za kimaandiko kwa ajili ya majukumu ya kifamilia na mahusiano.